

LAWYERS' ENVIRONMENTAL ACTION TEAM (LEAT)

*Research, Advocacy and Training on Environmental / Natural Resource Law and Policy and the
Promotion of Human Rights*
Website: <http://www.lead.or.tz>

Tel : +255 22 2780859
Fax : +255 22 2781098
Email : info@lead.or.tz
Website : <http://www.lead.or.tz>



Mazingira House, Plot No. 428
Mazingira Street, Mikocheni "B"
P. O. Box 12605
Dar es Salaam

TAARIFA KWA UMMA

TAMKO LA LEAT JUU YA ZUIO LA MATUMIZI YA MIFUKO YA PLASTIKI

Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo, (LEAT) imepokea kwa furaha kauli zilizotolewa bungeni na Waziri Mkuu, Ndugu Kassimu Majaliwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ndugu Januari Makamba, mnamo tarehe 10 Aprili 2019 wakati, Waziri Mkuu alipokuwa akifunga mjadala wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na wakati Ndugu Makamba alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Kaliua, Magdalena Sakaya (CUF), aliyetaka kujua ni lini mifuko ya plastiki, maarufu kama rambo, itapigwa marufuku kabisa nchini.

Kwa dhati kabisa, tunaipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchukua hatua ipaswayo. Imekuwa ni wito wa LEAT kwa muda mrefu wa kuitaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki nchini.

LEAT, kama wadau wa mazingira, tumekuwa tukipaza sauti na kupinga matumizi ya mifuko hii. Matumizi ya mifuko hii ni hatari kwa mazingira na viumbe vya baharini. Kumbukumbu zinaonesha kuwa siku za nyuma Serikali ilitoa kauli na baadaye Tangazo la Serikali (GN 137) la tarehe 6/10/2006 lililozuia kutengeneza, kuuza, kununua na kutumia mifuko ya plastiki. Lakini tangu kipindi hiko mpaka sasa mifuko ya plastiki imeendelea kuzalishwa, kuuzwa, na kuzagaa mitaani kutokana na ukweli kwamba kanuni hiyo iliruhusu kuendelea kutengenezwa mifuko ya plastiki yenye ujazo chini ya mikronzi 30 au milimita 0.03).

Aidha, matumizi ya mifuko ya plastiki umepelekea kukithiri kwa uchafuzi na uharibifu wa mazingira kama vile: kuzagaa kwake katika ardhi, uharibifu na uchafuzi wa vyanzo vya maji, vifo vya wanyama na viumbehai. .

Ikumbukwe kuwa kama matumizi ya mifuko na vifaa vya plastiki yataachwa kuendelea ifikapo mwaka 2030 kutakuwa na mifuko mingi baharini na kwenye maziwa na mito kuliko idadi ya samaki. Kwa sasa, takribani idadi ya mifuko trilioni 5.25 sawa na uzito wa tani 270,000 inaelea katika bahari,

Tafti zinaonyesha kuwa mifuko ya plastiki ni sumu kwa wanyama ambayo pia inapelekea kuathiri afya ya binadamu kutokana na wanyama hao kuwa kitoweo kwa binadamu. Takribani viumbe milioni 100 vya bahari hufa kila mwaka kwa kula mifuko ya plastiki.

Baadhi ya viumbe vya baharini kama kobe wamekutwa na kiasi kikubwa cha mifuko hii tumboni mwao kutokana na kushindwa kutofautisha mifuko na aina ya samaki (jellyfish) wanayokula.

Athari za mifuko ya plastiki zimedhihirika hasa katika ardhi kwani uchafuzi mkubwa unatokana na mifuko hii kupeperushwa na upepo na kukwama katika mitaro ya maji taka na maji safi. Hii hupelekea kutuama kwa maji katika mitaro mingi hasa katika jiji la Dar es salaam. Hali hii ndiyo chanzo kikubwa cha mafuriko kipindi cha msimu wa mvua, na kupelekea ulipukaji wa magonjwa ya kuhara na malaria kwani maji yaliyotua hutunza bakteria na wadudu kama mbu.

Mifuko hii pia ikitupwa katika madampo huchukua nafasi kubwa na hutumia takribani miaka 400 kuoza. Hivyo kusababisha kuendelea kuzagaa kwa mifuko hii katika mazingira.

Utengenezaji wa mifuko ya plastiki unasababisha changamoto kubwa katika mazingira kwani hutengenezwa na mafuta ya petroli. Hii hupelekea kiasi flani cha mafuta kila mwaka kuelekezwa katika uzalishaji wa mifuko. Utengenezaji wa mifuko hii huchangia katika kuongeza hewa ya ukaa ambayo husababisha mabadiliko ya tabia nchi.

LEAT inahimiza kuwepo na usimamizi na utekelezaji kamilifu wa zuio hili ili kuweza kupata matokeo chanya pamoja na kuboresha mazingira yetu. Zuiro hili lifanywe kwa umakini mkubwa na bila kurudi nyuma. Serikali ijifunze kutoka nchi tangulizi ambazo zilizuia matumizi ya mifuko hiyo kabla yetu. Mfano mzuri ni nchi ya Bangladeshi ambayo ilikuwa nchi ya kwanza duniani kuzuia matumizi ya mifuko ya plastiki mnamo mwaka 2002. Nchi nyingine ni: China, Israel, Afrika Kusini, Kenya, Uholanzi, Morocco, Rwanda, Mauritania, Sri Lanka, Papua New Guinea, Vanuatu, Albania, na Georgia. Aidha, Zanzibar, ambayo ni sehemu ya nchi yetu, ilipiga marufuku matumizi hayo miaka michache iliyopita.

Mwisho, LEAT inaitaka Serikali kuwa katika mstari wa mbele kupigania utunzaji na ulinzi wa mazingira ya nchi yetu ili Watanzania waweze kuishi katika mazingira safi na salama. Aidha, inawataka wananchi wote kuacha kutumia mara moja mifuko ya plastiki na kuchangamkia fursa ya kutengeneza vifungashio rafiki na mazingira na kutunza mazingira yao kwa ujumla kwa ustawi wao.

Imetolewa mjini Dar es Salaam leo siku ya Jumanne tarehe 16 Aprili 2019.



Dk. Rugemeleza A.K. Nshala
Mkurugenzi Mtendaji